## Video ya 1: Ukweli wa musingi ju ya Finland

**Hii ni video kwa ajili ya bakimbizi benye bameenda kuishi huko Finland**

**Je, Finland ni inchi ya namuna gani?**

- Finland ni inchi ndogo sana, inapatikana Kaskazini mu dunia katikati ya Uswidi na Urusi.
- Muji wake mukuu na mukubwa zaidi ni Helsinki, lakini manispaa nyingi inchini Finland ni kidogo sana na batu karibu elfu banaishi huko.
- Batu bote ba Finland ni karibu mamilioni 5.5.
- Finland ni inchi yenye amani yenye haki za batu banaheshimika.

**Je, Finland inakaa namuna gani?**

- Pande kubwa ya Finland imezungukwa na musitu na lacs, lakini pia kuna mamuji na manispaa muchache katika sehemu mbalimbali mu nchi.
- Mujengo ni muzuri na mametengenezwa sana.
- Inchini Finland kuna maeneo muchache enye batu bengi. Batu bana nafasi mingi yakuzunguka hao na maisha en general ni ya amani na ya mupango muzuri.
- Mamuji na mashambani ni safi na mametunzwa muzuri. Lazima wutupe takataka kwenye mapipa ya takataka tu na ni lazima kutupa takataka yako yote kwa kufata maelekezo.

**Je, batu ba Finland banasema lugha mugani?**

- Malugha officiel ya Finland ni Kifini na Kiswidi.
- Kuna baazi ya manispaa benye batu ba kusema Kiswidi bamejaa kuliko batu bengine.
- Batu bengi ba Finland banasema Kiingereza, lakini ili kujua Kifini na Kiswidi banapatikana shuleni na kazini.
- Kwa sababu ya batu ba inchi ya mbali kuhamia huko, kuna batu banaongezeka ba kusema Kirusi, Kiestonia, Kiarabu na malugha ingine ya kigeni.

**Je, hali ya hewa mu Finland iko namuna gani?**

- Kuna majira ine tofauti: kipupwe, kuchipua, kiangazi na vuli.
- Kipupwe iko na baridi na neje, lakini ndani mu nyumba na mujengo ya bato nyonso, iko joto muda yote mwaka muzima.
- Hata bakati baridi, batoto banenda mu shule na batu bazima banenda kazini.
- Bakati ba kuchipua, neje inayeyuka na musimu wa mumea kumea unaanza.
- Kiangazi ni kipindi mu joto, na kila kitu iko rangi ya kijani.
- Batoto ba shule na batu ba kazi bana likizo murefu bakati ba kiangazi.
- Bakati ba vuli, hali ya hewa inaanza kuwa baridi sana na mumea mingi inaanza kuangusha majani yawo.

**Je, wilaya ya kutawala iko namuna gani huko Finland?**

- Inchi imegawanywa katika mikoa, na kila mukoa umegawanywa katika manispaa.
- Manispaa inamaanisha sehemu ya kutawala yenye kupanga huduma ya batu bake. Inaweza kuwa muji mudogo au muji mukubwa.
- Kila mukoa inchini Finland iko na histoire tofauti na mutamaduni yawo wenyewe.
- Utaenda kwenye manispaa na kwa nyumba yako mwenyewe ya kupanga immediatement unapofika Finland.

**Je, matukio muhimu sana histoire ni mugani?**

- Kama ilivyo kwa mainchi mingi, Finland ilivamiwa zamani na kupigana vita.

- Finland ilikuwa sehemu ya Bokonzi ya Uswidi kwa mwaka 600 na baadae sehemu ya Nguya ya Urusi kwa mwaka 100, lakini Finland ilikuwa inafanya maamuzi yake peke yake.
- Finland ilipata uhuru mwaka 1917. Muda muchache baadae kulikuwa na vita ba benyewe kwa benyewe mwaka 1918.
- Bafini baliungana wakati balipigana na Umoja wa Kisovyeti katika Vita ya Pili ya Dunia.
- Zamani batu bengi ba Finland balikuwa na umasikini, njaa na hali duni ya maisha.
- Baada ya vita ya benyewe kwa benyewe, balitengeneza tena Finland na baada ya muda imekuwa mahali muzuri.
- Finland haijapigana vita na nchi ingine yoyote tangu 1945.
- Finland ilijiunga na Umoja wa Ulaya mwaka 1995.

**Je, ebongiseli ya siasa mu Finland iko namuna gani?**

- Finland ni Jamhuri ya Kidemokrasia.
- Rais ndiyo mukuu wa serikali inchini Finland.
- Mwanamuke na mwanaume bamewai kuchaguliwa kuwa mukuu ya inchi ya Finland.
- Bunge iko wabunge 200 banawakilisha vyama na mutazamo mingi tofauti ya kisiasa.
- Batu bote ba Finland zaidi ya miaka 18 bana haki ya kupiga kura.
- Batu ba inchi ingine bana haki ya kupiga kura baada ya miaka mbili ya kuishi inchini Finland.

**Je, sheria ya Finland inalinda haki ya batu namuna gani?**

- Katiba ya Finland inasema kila mutu anayeishi Finland ako na haki kama ya batu bengine na bote bako sawa bila kujali inchi yake, umri, jinsia, afya au sababu ingine.
- Bakimbizi ni batu ba jamii na bako na haki na kazi sawa kama batu bengine ba Finland.
- Wanawake na wanaume ni sawa inchini Finland. Kila mutu ako na haki ya kutoa maoni yake na uhuru wa kuvaa vile anataka.
- Hakuna mutu anaweza kuhukumiwa kifo au kuteswa.
- Batoto, bibi na bwana au mutu ingine hawezi kunyanyaswa; hawezi kuchapwa, kupigwa makofi, kuvurutwa nywele, au kunyanyaswa kwa njia ingine.
- Unyanyasaji wa kisaikolojia hairuhusiwi.
- Kukeketa wanawake na kunyanyasa batu habaruhusiwi kabisa.
- Inchini Finland, maafisa, pamoja na polisi, ni batu ba kutegemea sana na banaheshimika kwa sababu kazi yawo ni kusaidia na kulinda batu ba inchi. Kutokana na utafiti, 95% ya Bafini banafikiria polisi ni batu ba kuaminika.
- Hakuna sababu ya kuogopa afisa yoyote.
- Finland ni moja ya inchi yenye kiwango kidogo ya ufisadi duniani.

**Je, dini kuu inchini Finland ni gani?**

- Dini kuu ya Finland ni Ukristo na Bafini bengi bako kanisa la Kiinjili la Kilutheri.
- Dini inaonekana kama kitu ya kibinafsi na haina jukumu kubwa sana katika maisha ya batu.
- Idadi ya baislamu inaongezeka inchini Finland na kuna manyumba mingi ya kuswali katika manispaa kubwa kubwa.
- Kuna uhuru ya dini inchini Finland, yaani kila mutu ako na uhuru wa kuwa katika jumuiya ya dini na kufanya mambo ya dini, vilevile ako na uhuru wa kukataa dini yoyote.

**Je, jamii ya Bafini iko namuna gani?**

- Tangu kupata uhuru, Finland imepitia mabadiliko makubwa.
- Finland ilitoka uchumi duni ya kilimo na kubadilika kukuwa jamii ya teknolojia, mahali teknolojia, habari na huduma inafanya kazi muhimu katika kutengeneza utajiri ya inchi.

- Inchi na manispaa inahakikisha huduma ya kutosha ya kijamii na afya kwa batu bote ba inchi. Huduma hii inatoka kwa ushuru ya batu ba Finland.
- Batu bote ba inchi, pamoja na bakimbizi banalipa ushuru ili kudumisha mufumo ya ustawi mu Finland pamoja na elimu, afya, huduma ya miundombinu ya kijamii na ya bato nyonso.
- Kwa hivyo, ni muhimu kujifunza lugha ya Kifini au Kiswidi na kujitayarisha kusoma na kufanya kazi.
- Wanawake na wanaume ni sawa mu Finland na bote banatarajiwa kufanya kazi.
- Kuna wanawake bengi banafanya kazi kubwa katika siasa, kazini na maeneo ingine ya jamii.
- Tangu miaka ya 1990 Finland imeendelea kukuwa wa utamaduni mingi zaidi na batu ni ba mainchi na makabila mingi tofauti. Ingawa unaweza kukabiliana na xénophobie au ubaguzi wa rangi kama mahali pengine popote, Bafini bengi ni marafiki.

**Je, familia ba Finland ni namuna gani?**

- Familia ya musingi katika Finland kwa kawaida ya bazazi na batoto.
- Ingawa batu ba Finland kwa kawaida banaona bazazi au nyanya na babu kama familia ya karibu, mara mingi habaishi pamoja.
- Huko Finland, batu ba kijinsia kama vile ba jinsia moja, basagaji na batu ba kubadilisha jinsia bako na haki ya kukuwa kwa uhusiano.
- Ni kitu ya kawaida na banakubalika kwa batoto ba miaka 18 kuhama na kuishi mbali na bazazi.
- Watoto sio lazima basaidie bazazi na pesa.

**Je, ni nini muhimu kwa batu ba Finland?**

- Batu ba Finland banaheshimu kuweka siri, uaminifu na kotosa ngonga.
- Kwa jumla, Bafini banapenda afya njema, familia, kazi na uwezo wa kujiendeleza kupitia kufanya shughuli ya wakati ya mapumuziko.
- Bafini bengi banapenda mashughuli ya inje kama vile kutembea musituni, kuendesha baiskeli, kuteleza kwa neje, kuvua samaki na kuogelea katika lacs au bahari.
- Batu ba Finland banapenda kuoga ndani ya sauna. Sauna ni mahali ya kawaida ya uoga. Sauna inaweza kupatikana katika manyumba ya batu bengi na banatumiwa mara nyingi.
- Muchezo ni muhimu katika tamaduni ya Finland. Bafini banatambuliwa duniani katika muchezo mingi, mingimingi hockey ya galasi, na kushinda mashindano mingi ya dunia.
- Batu pia banapenda kufanya muchezo mingi ili kutunza afya na maisha yawo.
- Kwa mopoti-mbangu mudogo mwenye talanta na wa kufanya bidii, inawezekana kuwa mopoti-mbangu professionel ba Finland.

**Je, ni nini inafanya Finland kuwa inchi ya teknolojia ya juu?**

- Mambo mingi katika jamii ya Finland iko dijitali na batu bengi banatumia vitu ya teknolojia kama smart phone, laptop na tablet.
- Vitu tofauti ya electronique inatumiwa kila siku na shughuli mingi ya kila siku inafanywa na smart phone, kwa mufano kulipa bili, kununua vitu na miadi ya huduma za bato nyonso.
- Katika taaluma nyingi, ni lazima kutumia teknolojia ili kufanya mambo ya kazini.
- Kuna kozi ya kujifunza hii mambo na ni muhimu kujifunza kutumia vitu ya dijital.
- Katika familia mingi, batoto banatumia hii vitu na teknolojia inaendelea kutumiwa pia shuleni na walimu.

## Video ya 2: Maisha huko Finland

**Hii ni video kwa ajili ya bakimbizi benye bameenda kuishi huko Finland**

**Je, nitasafiri namuna gani kuenda Finland?**

- Ukichaguliwa kama mukimbizi inchini Finland, utapewa idhini ya makazi ya kudumu miaka inne na unaweza kupata ingine mupya baadae.
- Utapatiwa idhini yako ya makazi na makaratasi ya kusafiri kabla ya kusafiri.
- Serikali ya Finland itapanga na kulipia safari yako ya Finland.
- Utasafiri kwenda Finland na ndege na unaweza kubadilisha ndege njiani.
- Utasaidiwa katika uwanja ya ndege.
- Unaweza kuchukua mufuko moja tu ya kilo 20 kwa ndege na kuongeza muzigo ya mukono na isipite kilo 8.

**Je, nini itafanyika nikifika Finland?**

- Mipango yako ya kusafiri haitaanza mpaka wakati manispaa moja inchini Finland itakukaribisha baada ya kuweka nyumba tayari kwa ajili yako.
- Hautaishi kwa kituo ya bakimbizi, lakini katika nyumba ya kukodisha ambayo ni nyumba yako mwenyewe.
- Huko Finland utasafiri moja kwa moja kutoka uwanja ya ndege ya Helsinki kwenda manispaa yako mupya kwa ndege, kwa basi au kwa gari.
- Baada ya kufika, utapatiwa funguo ya nyumba yako.
- Viongozi na mashirika ya manispaa yako batakushauri kutoka siku ya kufika, lakini lazima ukuwe na bidii ya kujifunza mufumo mupya pia wewe mwenyewe.

**Je, nitabeba nini nikienda Finland?**

- Lazima ubebe makaratasi yote ya kitambulisho kama pasipoti, kadi za kitambulisho, leseni ya kuendesha gari, cheti ya kuzaliwa, kitabu ya familia nk.
- Chukua makaratasi yote muhimu zaidi ya afya kama vile uchunguzi ya daktari, matibabu na histoire yako ya matibabu.
- Leta pia makaratasi muhimu zaidi ya elimu kama vyeti, digrii na diploma.
- Leta vyeti ya histoire yako ya kazi kama inapatikana, yenye inaonyesha umefanya kazi wapi, kazi ile ulifanya, na kwa muda gani umefanya kazi.
- Kama inawezekana, tafsiri hiyo makaratasi kwa Kiingereza kabla ya kuenda Finland.
- Ni muzuri kuleta pia mapicha yako muhimu, vitu ndogo ndogo ya kukumbukwa na vitu yako ya thamani huko Finland.

**Je, nitaishi namuna gani kama sijui lugha ya Finland?**

- Ni muhimu kuanza kujifunza mara moja lugha ya Finland, baada ya mahojiano yako ya kuchaguliwa ya bakimbizi.
- Viongozi na mashirika ya manispaa yako batakusaidia na kukushauri katika kuandaa maisha yako ya kila siku kutoka siku ya kufika, lakini lazima ukuwe na bidii pia wewe mwenyewe.
- Mutazamo muzuri itakusaidia wakati wa kutulia inchini Finland.
- Viongozi wa Manispaa batahakikisha umesajiliwa katika ofisi ya usajili katika manispaa hiyo ambayo utakuwa unaishi.
- Baada ya kufika, wutakuwa na haki ya kuwasiliana kupitia mukalimani, lakini ni muhimu kuanza mara moja kusoma Kifini au Kiswidi, kwa sababu lugha hizi banatumiwa katika jamii ya Finland na huduma ya ukalimani ni muchache sana.

- Hutakikani kutumia batoto bako kama mukalimani ingawa banaweza kujifunza lugha mupya haraka.

**Je, kwa nini inchi na manispaa bananisaidia?**

- Unatarajiwa kusoma taaluma na kujisaidia pamoja na familia yako kwa kufanya kazi. Hii ni kwa wanaume na wanawake.
- Finland in inchi ya kusaidia batu na manispaa yako inakusaidia kujumuika kabla ya kuweza kujisimamia mwenyewe.
- Jamii pia banasaidia bagonjwa, batu baliostaafu na wale ambao habawezi kujitegemea peke yao na banahitaji musaada zaidi.
- Mufumo ya kusaidia batu banatoka kwa pesa ya ushuru yenye imekusanywa kutoka kwa batu bote na makampuni yote.
- Batu bote ba Finland lazima balipe ushuru, hata kama unasoma, unafanya kazi, wewe ni mugonjwa ama haufanyi kazi.
- Ushuru inatumiwa kwa hosipitali, huduma ya afya, huduma ya kijamii, elimu na shule, huduma ya kutunza batoto muchana n.k.
- Kama mukazi wa manispaa, unastahili kupata huduma ya musingi, kama vile elimu, afya na huduma ya kijamii, kama Bafini.
- Wakati huo huo, lazima ufate sheria na kanuni za Finland kama Bafini.

**Je, batu banaweza kubadilisha manispaa?**

- Ni ngumu kuhamia manispaa ingine kabla ya kuweka pesa ya kutosha kwa ajili ya gharama na lazima ukuwe unajua jinsi ya kufanya hivyo peke yako.
- Batu banaishi Finland banaweza kuhama kutoka eneo moja kwenda ingine, lakini ukifika inchini Finland kama mukimbizi, inashauriwa ukae katika manispaa ya nyumbani kwako angalau miaka tano ya kwanza.
- Manispaa ya nyumba yako imejitayarisha kukukaribisha na kukupatia mahali pa kuishi na huduma na musaada muhimu.
- Ukihama haraka sana, manispaa mupya inaweza kukosa kukupatia huduma ya kukujumuisha huko ambayo ni ya kibinafsi na ya muhimu sana.
- Hakuna nyumba ya bei ya chini na sio rahisi kupata nyumba mupya.
- Kama utahama, lazima utalipa gharama wewe mwenyewe.

**Je, ni rahisi kuchanganyana na batu bengine?**

- Kuhamia inchi mupya inaweza kuwa ngumu haswa wakati wa mwanzo. Inachukua muda na juhudi kuchanganyana na batu katika jamii mupya, lakini mutazamo muzuri itakusaidia sana.
- Ni muhimu kuwa na hamu na kuvutiwa na inchi yako mupya.
- Hata kama kutakuwa na mabadiliko mengi katika maisha yako ya kila siku, lazima ukuwe tayari kujifunza mambo mupya na ukuwe na ujasiri wa kujua batu ba Finland.
- Kujua lugha na mitandao ya kijamii itakusaidia kuchanganyana na batu. Unapoendelea kujifunza Kifini au Kiswidi, itakuwa rahisi kujua batu ba Finland na kupata marafiki.
- Inasaidia sana kama unafata sheria na ushauri ya viongozi.
- Kumbuka ni muzuri kukuwa mutu ya kuchangamuka, kwa mufano kwa kushiriki katika shughuli tofauti na kuanza mazungumzo na batu bapya.

**Je, nitapata nyumba ya kuishi namuna gani?**

- Huko Finland utaishi katika nyumba ya kukodisha ambayo manispaa yako inapanga kwa ajili yako.

- Manyumba mingi ya manispaa imepangwa katika manyumba ya gorofa
- Manyumba inaweza kuwa tofauti kwa size na mutindo, lakini mingi iko na shambre sawa ndani ya nyumba, ambayo ni bafu, jikoni, salon, shambre ya kulala na shambre ya batoto, ikiwa inahitajika.
- Nyumba iko na mahali moja ya kuleta joto na mwaka muzima iko joto kwa nyumba.
- Kuna umeme na maji ndani ya nyumba.

**Je, nyumba ya kukodisha iko na vitu ndani?**

- Kutakuwa na vitu ya musingi tayari wakati utafika, kama vitanda au magodoro, shuka, fanicha kazaa na vyombo ya jikoni.
- Hakutakuwa na televisheni au simu kwa hiyo nyumba. Baadae unaweza kuokoa pesa ya kununua vitu unahitaji kwa nyumba yako.
- Batu ba Finland banapika chakula sana kwenye majiko ya umeme.
- Kuna friji na wakati ingine pia kuna freezer ndani ya manyumba.
- Manispaa yako itakupatia ushauri ya jinsi ya kutumia hii vitu.

**Je, naweza kuvuta sigara ndani ya nyumba?**

- Kawaida hakuna ruhusa ya kuvuta sigara ndani ya nyumba yako na majengo ingine.
- Hakuna ruhusa pia ya kuvuta sigara ndani ya majengo na magari ya bato nyonso.
- Hakuna ruhusa ya moto inawaka ndani ya nyumba.

**Je, mutu anaweza kunywa maji ya mufereji?**

- Maji ya mufereji huko Finland ni safi sana na unaweza kunywa kutoka mufereji bila kuchemusha.
- Unaweza kupata maji ya moto na baridi kutoka kwa mufereji na shower yako.
- Lazima ulipe maji ile unatumia kwa nyumba, kwa hivyo inashauriwa usitumie maji mingi kupita kiasi.

**Je, nitasafiri namuna gani ndani ya manispaa?**

- Katika manispaa mingi kuna mabasi ya kuaminika ya bato nyonso.
- Katika manispaa ndogo huduma ya musingi kawaida iko karibu na manyumba ya kukodisha, kwa hivyo unaweza kufikia huduma yote muhimu kwa miguu.
- Kuendesha baiskeli pia ni njia salama na ya bei ya chini ya kusafiri kama huendi mbali.
- Kutembea ni muzuri kwa afya na kawaida batu hutembea umbali murefu kama kilomita 2-5 kwenda kazini au shuleni.
- Mabasi na gari moshi inatoa huduma ya safari ya mbali. Kwa kuongezea, ndege ya ndani ya inchi inapatikana, lakini bei iko juu.
- Huduma ya usafiri ya kitaifa, region na mitaa imeundwa kupatia abiria huduma ya kuaminika, salama na kamili. Kutumia usafiri wa bato nyonso ni rahisi kuliko kuwa na gari ya kibinafsi.
- Teksi ni pesa mingi sana huko Finland, kwa hivyo tumia tu kama ni muhimu sana.

**Je, usafiri ya bato nyonso ni salama kwa familia yangu?**

- Usafiri ya bato nyonso ni salama kwa kila mutu.
- Wanawake banaweza kutumia usafiri wa bato nyonso peke yao.
- Batoto banaweza kutumia usafiri wa bato nyonso peke yao kwenda shule na wakati wa shughuli ya mapumziko.

- Kama mutu anasahau njia au mahali ya kushuka, madereva na abiria bengine banaweza kusaidia.
- Kuna programu ya mtandaoni ya kutoa mwongozo, ramani na ratiba ya njia ya usafiri wa bato nyonso.

**Je, nitanunua chakula namuna gani?**

- Batu ba Finland bananunua chakula na vitu ingine kutoka kwa maduka makubwa.
- Siku hizi kuna maduka mingi inchini Finland ya kuuza aina tofauti ya chakula iliyoletwa inchini kutoka inchi za Kiarabu, Asia na Afrika.
- Katika musimu ya joto, masoko inauza mboga mupya na bizaa ingine kama uyoga na matunda kutoka musituni. Masoko pia ni mahali ya batu kukutana.
- Unaweza kuchagua matunda ya musituni na uyoga kutoka kwa musitu.

**Je, nitaweza namuna gani kukuwa na pesa ya kutosha kununua vitu yote muhimu kwa nyumba yangu na familia?**

- Mwanzoni utapata musaada ya pesa kwa ajili ya gharama ya musingi ya kuishi kupitia mufumo ya kijamii. Kiasi ya musaada ni kulingana na sheria.
- Musaada yako inatosha gharama ya musingi na inalipwa mara moja tu kwa mwezi.
- Si muzuri kuchukua mukopo ya kulipa gharama yako.
- Bei ya vitu huko Finland iko juu kabisa. Ni muhimu kupanga matumizi ya kila mwezi ndani ya familia.
- Ni kawaida kununua nguo, fanicha, baiskeli na vitu ya batoto katika duka ya mutumba ambapo bei iko chini sana.
- Ubora katika maduka ya mutumba inaweza kuwa ya juu sana na kuna aina mingi ya bizaa.
- Siku hizi kununua na kuuza nguo na viatu kwenye mutandao ni kitu ya kawaida.

**Je, Finland inatumia sarafu gani?**

- Sarafu ya Finland ni euro. Ni sarafu ambayo inatumika na inchi mingi ya Jumuiya ya Ulaya.
- Finland ilianza kutumia euro 2002.

**Je, ninaweza kutumia pesa wakati wa kununua vitu?**

- Malipo inaweza kufanywa na pesa au kadi ya benki. Hata hivyo, batu bengi sana banatumia kadi kama njia ya malipo.
- Unahitaji akaunti ya benki ili kupata kadi ya benki.
- Ni muhimu kwa kila mukimbizi mutu muzima kufungua akaunti yake ya benki.
- Wanaume na wanawake bana akaunti yao tofauti ya benki.

## Video ya 3: Huduma ya watoto, elimu na haki ya musingi kwa batoto ba Finland

**Hii ni video kwa ajili ya bakimbizi benye bameenda kuishi huko Finland**

**Je, Finland ni inchi muzuri kwa kulea batoto?**

- Finland inatoa huduma bato nyonso kwa bakazi bote.
- Wanawake ba mimba na batoto ba kila umri banapata huduma maalumu katika kliniki ya afya.
- Huko Finland, sheria hairuhusu batoto kusoma na kuwacha shule.
- Haki ya musingi kwa batoto ni pamoja na haki ya afya, elimu, maisha ya familia, muchezo, maisha bora na kulindwa kutokana na mateso na kuumizwa.

**Je, jinsi ya kulea batoto ni tofauti huko Finland?**

- Bazazi bote duniani banataka maisha bora kwa batoto yao. Lakini tabia ingine ya kulea batoto inaweza kubadilika ukifika Finland.
- Mahitaji ya batoto lazima isikilizwe na ni lazima kuishi katika mazingira salama na kuwa na uhusiano muzuri, wa karibu.
- Wasichana na wavulana lazima bafanyiwe mambo sawa, na kufurahia haki sawa katika maisha yao yote.
- Lazima utunze maisha ya batoto yako kabisa hadi batoto bako bakue mutu muzima.
- Katika sheria ya Finland, batoto banakuwa mutu muzima banapofika miaka 18.
- Kama uko na changamoto ya kulea au uhusiano wa familia, unaweza kuomba musaada kutoka kwa huduma ya kutunza batoto muchana, shule au huduma ya ushauri ya familia ya manispaa.

**Je, ninaweza kumuchapa mutoto yangu?**

- Huko Finland kuchapa mutoto ni makosa.
- Huwezi kuazibu batoto kwa kupiga kofi au kuvuruta nywele. Kunyanyasa batoto kwa njia yoyote ni makosa.
- Kuna njia tofauti ya kulea na kuazibu mutoto ambayo inafanya kazi muzuri.
- Hii njia tofauti inaweza kujadiliwa na bafanyikazi ba kijamii na ba afya, huduma ya kutunza batoto muchana na shule.

**Je, nani anachunga batoto muchana kama bazazi banasoma au bameenda kazini?**

- Manispaa yote inatengeneza elimu ya batoto badogo katika mahali ya kutunza batoto muchana kwa batoto chini ya miaka saba na shule ya mapema kwa batoto ya miaka sita.
- Bazazi bote banaweza kufanya kazi au kusoma wakati batoto bako katika mahali ya kutunza batoto muchana.
- Huko mahali ya kutunza batoto muchana hao banacheza na kujifunza stadi tofauti muhimu wakati wa kuanza shule ya musingi. Walimu ya mahali ya kutunza batoto muchana bamesoma kabisa.
- Batoto ba batu ba inchi ingine banajifunza Kifini au Kiswidi haraka sana wakati wanachanganyana na batoto bengine mahali ya kutunza batoto muchana.
- Batoto ba mahali ya kutunza muchana banapatiwa chakula yote muhimu.
- Batoto banaweza kuanza utunzaji ya muchana hata kabla ya mwaka mumoja ikiwa bazazi banafanya kazi au banasoma.
- Ni muzuri mutoto yako kuanza utunzaji wa muchana kama amechelewa sana, akiwa na miaka tatu ili ajifunze lugha ya Kifini au Kiswidi.

**Je, masomo ya batoto badogo ni ya bure?**

- Kuna pesa ya kulipa kutegemea mapato ya familia yako na batoto yako ni ngapi.
- Kawaida batu banalipa elimu ya batoto badogo kama banafanya kazi na banapata mushahara ya kutosha.
- Batu ba mapato kidogo habalipi kitu, lakini batoto yao banapata huduma sawa.

**Je, mutoto anaenda shule na miaka ngapi huko Finland?**

- Batoto banaanza darasa ya kwanza ya elimu bakiwa miaka saba.
- Batoto bote inchini Finland lazima baende shule.
- Elimu ya shuleni kawaida inadumu miaka tisa katika umri wa miaka 7-16.

- Batoto benye habasemi Kifini au Kiswidi banapokea musaada zaidi katika kujifunza hiyo lugha.

**Je, siku ya shule katika shule ya musingi iko namuna gani?**

- Siku ya shule inaweza kuanza wakati tofauti kwa siku tofauti. Kwa kawaida, siku ya shule inaanza saa mbili au saa tatu asubuhi kutoka Jumatatu hadi Ijumaa.
- Katika siku ya shule kuna masomo tofauti kama lugha, hesabu, biolojia, histoire na michezo.
- Batoto banacheza inje wakati wa kupumuzika.
- Batoto bote banakula chakula ya muchana ile joto huko shuleni.
- Walimu banaweza kupatia batoto kazi ya nyumbani kila siku.
- Siku ya shule inaisha kawaida kati ya saa sita na saa nane jioni.

**Je, kazi ya bazazi ni nini kwa masomo ya batoto?**

- Kama muzazi lazima kuangalia kwamba batoto bako banaenda shule kwa masomo yote kila siku.
- Lazima ujulishe shule mara moja kama batoto bako habataenda shule kwa sababu ya ugonjwa au sababu ingine.
- Lazima uangalie kuwa batoto bako banamaliza kazi ya nyumbani waliyopewa na walimu.
- Shule na bazazi ba Finland banawasiliana mara kwa mara kuhusu maendeleo ya wanafunzi.

**Je, batoto banaweza kufanya nini wakati ba kupumuzika?**

- Ni muhimu kwa batoto kufanya mambo ya wakati ya kupumzika kwa sababu banaweza kujifunza lugha na kupata marafiki ba Finland.
- Kuna mambo tofauti ya kuchagua kufanya wakati wa kupumuzika kwa ajili ya batoto huko Finland.
- Iko nafasi ya kucheza muchezo, dansi, muziki, sanaa ya kuchora au theatre, kozi za kupika, na ingine mingi.
- Shule mingi, vituo ya vijana, mashirika na maktaba za bato nyonso inapanga shughuli tofauti ya wakati ba kupumuzika kwa ajili ya batoto.

**Je, hii mashughuli ni ya bure?**

- Shughuli ingine kama vilabu ya muchezo, lazima kulipa pesa, lakini pia kuna shughuli mingi ya bure kabisa.
- Familia inaweza kufurahia shughuli mingi ya wakati wa kupumuzika pamoja bila gharama yoyote kama kutembelea uwanja ya muchezo, maktaba ya bato nyonso, na sherehe ya kitamaduni na muchezo.
- Ni muhimu familia kutumia wakati pamoja na kupeleka batoto yao kucheza.

## Video ya 4: Fursa ya elimu na maisha ya maana kwa vijana

**Hii ni video kwa ajili ya bakimbizi benye bameenda kuishi huko Finland**

**Je, mufumo ya elimu iko namuna gani huko Finland?**

- Mufumo ya elimu ya Finland inajulikana kwa ubora ya juu sana. Inatoa fursa sawa ya elimu kwa kila mutu, haijalishi mtu ako na miaka ngapi.
- Elimu ya Finland iko na shule ya musingi (darasa ya 1-6) na shule ya sekondari (darasa ya 7-9), elimu ya juu ya sekondari na chuo kikuu. Masomo yote ni ya bure.

- Shule ni kwa batu ba chini ya miaka 18.
- Manispaa yako itapanga mahali ya kusoma katika shule ya mutaa yako na utapatiwa musaada ya kujifunza Kifini au Kiswidi.
- Mwalimu wako atachambua ni darasa gani inakufaa zaidi, kwa kuzingatia masomo yako ya zamani na umri yako.
- Ukifika Finland na miaka 17 au zaidi, unaweza kusoma elimu yote ya shule ya sekondari katika shule ya elimu ya juu ya sekondari ya mutu muzima.
- Huko Finland masomo imetengenezwa kwa ajili ya wanafunzi tofauti ili kila mwanafunzi aweze kumaliza masomo yake na kuingia chuo kikuu au maisha ya kufanya kazi.

**Je, ninaweza kusoma kwa Kifini au Kiswidi?**

- Baada ya darasa ya kuandaa ya mwaka mumoja au musaada inayofanana na hiyo ya kupata mambo muhimu ya lugha, utapokea musaada kwa Kifini au Kiswidi wakati wote wa masomo.
- Kiingereza inafundishwa shuleni kama lugha ya pili na kuna lugha mingi ingine ambayo unaweza kusoma, lakini shule itachagua.

**Je, ninaweza kufanya kazi baada ya shule ya sekondari?**

- Sio kawaida au rahisi kuanza kufanya kazi baada ya shule ya sekondari.
- Kuna kazi muchache tu kwa batu bila elimu. Kwa hivyo, unashauriwa kusoma zaidi huko Finland.
- Baada ya shule, unaweza kuingia elimu ya juu ya sekondari kwa masomo zaidi, au unaweza kusoma katika chuo ya ufundi. Masomo yote mbili itachukua mwaka tatu.
- Baada ya kumaliza masomo ya ufundi, unaweza kuanza kutafuta kazi au mahali ya kufanya mazoezi ya kazi.
- Tayari wakati ya masomo, kuna muda mingi ya kufanya mazoezi ya kazi, na hapo unaanza kuzoea kazi.
- Kuna nafasi mingi ya wewe kufanya kazi ya muda mufupi wakati wa mapumuziko yako na likizo ya shule ili kupata pesa ya mfukoni.
- Kutoka mwaka 15 unaweza kusaini kontra ya kazi wewe mwenyewe. Kabla ya hapo kontra lazima itiwe saini na muzazi.

**Je, ninaweza kufanya nini wakati wa kupumuzika?**

- Manispaa na mashirika tofauti inatoa nafasi mingi ya shughuli ya wakati wa kupumuzika kwa vijana na mingi ni ya bure.
- Unaweza kuchagua mwenyewe aina ya shughuli ya wakati ya kupumuzika kutoka aina tofauti ya muchezo hadi muziki, dansi, sanaa, shughuli ya inje na kazi ya kujitolea.
- Kuna nafasi wazi na uwanja kwa muchezo ya nje ambayo inaweza kutumiwa na mutu yoyote.
- Maktaba mingi ya bato nyonso iko na maeneo maalumu kwa vijana kupumuzika na kucheza muchezo na kukutana na vijana bengine baada ya masaa ya shule na jioni.
- Unaweza kuomba vitabu kwa lugha tofauti bila gharama yoyote kutoka kwa maktaba yako ya bato nyonso.

**Je, uhusiano ya mapenzi na ndowa iko namuna gani huko Finland?**

- Vijana na batu bazima banajuana kwa kuchumbiana. Hii inapatia batu ba kupendana nafasi ya kujuana.
- Si lazima kuchumbiana kufanya uhusiano ya ndowa.
- Huko Finland, ni kawaida kuwa na uhusiano wa mapenzi kabla ya ndowa.

- Umri ya chini wa inchi kwa ajili ya ndowa ni 18 kwa jinsia yote mbili.
- Wanawake na wanaume bana haki ya kuchagua ni nani banatamani kuchumbia na kuowa; banaamua benyewe banataka kuishi na nani.
- Hakuna mutu anaweza kulazimishwa kuchumbiana au ndowa.
- Unaweza kuazibiwa na sheria ukilazimisha mutu kuowa, awe ni mwanaume au mwanamuke.
- Huko Finland unaweza kuwa na bwana au bibi mumoja tu wakati mumoja.
- Huko Finland, mutu yoyote anaweza kupata talaka na haitaji kutegemea mwenzake wa zamani kwa musaada ya pesa.

**Je, uhusiano ya kimapenzi inaruhusiwa kabla ya ndowa?**

- Wasichana na wavulana banafanya urafiki na kushirikiana kwa uhuru hata na jinsia tofauti. Hata hivyo,kuchumbiana haimaanishi kwamba vijana wakuwe na uhusiano ya kimapenzi.
- Ni halali na inakubalika kwa banandoa badogo kuishi pamoja na kuwa na uhusiano ya kimapenzi kabla na hata bila kuoa.
- Umri ya kukubali mambo ya ngono huko Finland ni miaka 16.
- Hii njo umri ya chini kabisa ya mutu kuonekana kutosha kisheria kuweza kukubali kushiriki katika mambo ya ngono.
- Kila mutu huko Finland ako na haki ya kisheria ya kumukataa mutu mwingine kumushika kwa mwili. Hakuna mutu, hata mupenzi wa ndowa, anaweza kulazimishwa kufanya ngono bila kukubali.

**Je, ninaweza kuanza familia na mutu ya Finland?**

- Uko na huru kuanzisha familia na mutu yoyote unayesikilizana nayeye na kukubaliana kuhusu hiyo uhusiano.
- Batu ba inchi tofauti kufanya ndowa na kuanzisha familia inaongezeka huko Finland.
- Bafini banachagua bapenzi yao benyewe na hakuna ruhusa inahitajika kutoka kwa bazazi au familia.
- Kabla ya kuanzisha familia, ni muhimu kwamba nyinyi wawili mujadiliane kabisa kuhusu maadili, matamanio ya baadae, hamu ya kupata batoto na maneno ingine muhimu ambao itaathiri maisha ya ndowa.
- Bapenzi banaweza kuuliza maoni ya familia yao, lakini familia au bazazi lazima baheshimu haki ya mutu binafsi ya kuchagua mupenzi wake.

**Je, ninaweza kuteswa au kubaguliwa kwa sababu ya inchi yangu na mutazamo tofauti?**

- Kuteswa na kubaguliwa ni makosa inchini Finland na kila mutu ni sawa katika sheria ya Finland.
- Katika mashule na huduma yote ya bato nyonso, kuteswa na kubaguliwa ni makosa kabisa.
- Ikiwa wewe mwenyewe uko tayari kukutana na batu bapya na kujaribu kutumia Kifini au Kiswidi, itakuwa rahisi kuchanganyana na Bafini..
- Shule, burudani na sherehe ya vijana ni nafasi muzuri ya kupata marafiki bapya.

## Video ya 5: Elimu na maisha ya kufanya kazi ya batu bazima

**Hii ni video kwa ajili ya bakimbizi benye bameenda kuishi huko Finland**

**Je, hatua ya kwanza baada ya kufika Finland ni gani?**

- Kama wewe ni mutu muzima mwenye afya muzuri na uko na miaka 17-64, lazima ujisajili katika huduma ya ajira kwa bato nyonso kama mutu asiye na kazi ambaye anatafuta kazi.
- Viongozi na washauri batakuongoza kupitia hii mambo yote.
- Ujuzi yako ya lugha na kazi yako ya zamani itaangaliwa, na utapata mupango ya kibinafsi ya kuchanganyana na batu.
- Ofisi ya kazi itakuandikisha katika kozi ya kuchanganyana na batu ya kukupatia ujuzi wa lugha, kuelewa jamii ya Finland na maisha ya kufanya kazi. Pia utafanya mazoezi ya kazi.

**Je, itakuwaje kama siwezi kufanya kazi?**

- Kama hutazingatiwa kuwa na uwezo wa kufanya kazi, kama vile walemavu, batu zaidi ya miaka 64, mama ya kuchunga batoto badogo nyumbani nk. hauitaji kujiandikisha katika ofisi ya kazi.
- Kama wewe ni wa hii kikundi, unatayarisha mupango yako ya kuchanganyana na batu pamoja na ofisi ya kijamii ya manispaa yako.
- Mupango wa kuchanganyana na batu itakuongoza kupata kozi muzuri ya lugha na shughuli ingine yenye maana kama vile vikundi tofauti ya kushughulika.
- Hata kama huwezi kuingia katika maisha ya kufanya kazi, ni muhimu sana kusoma lugha hiyo mupya na kufahamu jamii ya Finland.
- Unatarajiwa pia kutunza afya na maisha yako.

**Je, itakuwaje kama sijui kusoma au kuandika?**

- Kuna kozi maalumu ya kuchanganyana na batu kwa wale basiojua kusoma na kuandika.Hakuna haja ya kusoma au kuandika kabla ya kufika Finland au unaweza kusoma au kuandika kwa lugha yako peke yake.
- Kozi ya batu basiojua kusoma na kuandika inaenda polepole ili kila mutu aweze kujifunza ujuzi wa musingi wa kusoma.
- Baadae unaweza kujiunga na kozi ya juu zaidi ya kuchanganyana na batu.

**Je, batu bazima ba inchi ingine benye hawajamaliza shule yao banaweza kuenda shule?**

- Kama hujamaliza shule katika inchi yako na bado wewe ni mudogo, unaweza kujiandikisha katika shule ya elimu ya juu ya sekondari kwa batu bazima.
- Huduma za kazi kwa bato nyonso itatoa miongozo zaidi na kukusaidia kujiandikisha katika kozi ambayo inafaa zaidi kwako.

**Je, naweza kuanza kufanya kazi mara moja baada ya kufika inchini Finland?**

- Kama mukimbizi unapatiwa kibali ya makazi na haki ya kufanya kazi unapofika Finland. Haki yako ya kufanya kazi imeandikwa katika kadi yako ya kibali ya makazi.
- Unaweza kufanya kazi ya muda mufupi pamoja na masomo yako ingine.
- Hata hivyo, huko Finland, ni ngumu kupata kazi bila cheti rasmi iliyopatikana kutoka kwa masomo na ustadi ingine muhimu.
- Ni muhimu sana kujifunza ustadi ya musingi katika lugha ya Kifini au Kiswidi. Ni muhimu kuanza kujifunza maneno ya musingi hata kabla ya kufika Finland.
- Unaweza kupata kazi kupitia huduma ya kazi ya bato nyonso na ya kibinafsi au kwa kuwasiliana na waajiri moja kwa moja.
- Kuna kazi ya muda mufupi na ya muda yote. Masaa ya kawaida ya kufanya kazi ni masaa nane kwa siku.

**Je, ni aina gani ya kazi inapatikana katika soko ya kazi ya Finland?**

- Ustawi ya jamii, huduma ya afya, elimu ya batoto badogo na kusafisha ni kazi inayohitajika sana kwa wafanyikazi katika sehemu tofauti ya Finland.
- Pia kuna nafasi muzuri ya kazi katika ujenzi, kazi ya mutambo, upishi, misitu na usafirishaji.
- Kujua Kifini au Kiswidi ni muhimu katika kusoma shuleni na maisha ya kufanya kazi.

**Je, ninaweza kuanzisha biashara yangu mwenyewe huko Finland?**

- Kuwa mutu ya biashara ni njia moja ya kupata mapato yako mwenyewe inchini Finland.
- Kuna batu ba biashara ba inchi ingine baliofanikiwa, kwa mufano katika upishi, kuuza maduka, kuuza manyumba, ujenzi, usafirishaji na huduma ya kijamii.
- Kabla ya kuanzisha biashara, lazima ujuwe sheria ya Finland, mufumo ya ushuru, mazingira ya biashara na mahitaji ya kuanza biashara.
- Kujua lugha ya Kifini ni muhimu katika shughuli ya biashara.
- Unaweza kupokea musaada ya pesa kwa wakati ya kwanza ya kuanzisha biashara ikiwa mupango yako ya biashara imekubaliwa na huduma ya kazi.

**Je, ninaweza kusoma taaluma huko Finland namuna gani?**

- Kama tayari uko na digrii, unaweza kugundua jinsi ya kuhamishiwa kwa digrii kama yako huko Finland. Mara mingi utaulizwa kufanya masomo ya kuogezea huko Finland.
- Machuo mingi ya ufundi huko Finland inatoa aina mingi ya masomo ya ufundi na mupango ya mafunzo, na kupatia watu vyeti kwa aina tofauti ya kazi.
- Masomo inachukua kawaida miaka mbili hadi tatu.
- Machuo ya ufundi inatoa masomo ya kuongezea ya lugha na musaada kwa batu ambao lugha yao ya mama sio Kifini au Kiswidi.
- Kuna aina tofauti ya machuo ingine ya elimu ya juu, kama vyuo vikuu ya sayansi na vyuo vikuu.
- Huko Finland, elimu yote ya juu ni ya bure.

**Je, wanawake banaweza kufanya kazi ya namuna gani huko Finland?**

- Huko Finland ni kawaida kabisa kwa wanaume na wanawake kufanya aina yoyote ya kazi.
- Kwa mufano, wanaume banaweza kuwa walimu ya mahali ya kutunza batoto muchana au wauguzi na wanawake bengi banafanya kazi ya mukono au madereva ya mabasi.
- Wanawake bote banatarajiwa kusoma taaluma na kuingia katika maisha ya kufanya kazi.
- Mufumo wa utunzaji batoto muchana inasaidia wanawake kupata kazi ya kudumu hata kama bako na batoto badogo.

**Je, kama mama ya familia pia anafanya kazi, ni nani anatunza nyumba?**

- Huko Finland majukumu ya bazazi na ya nyumbani imegawanywa sawa kati ya wanaume na wanawake.
- Bazazi bawili banafanya kazi ya kupika, kusafisha, kununua vitu kwa duka na kutunza batoto.
- Wakati kila mutu ya familia anaenda shule na kufanya kazi, majukumu ya nyumbani inahitaji kugawanywa kwa usawa kati ya batu bote ba familia.
- Katika mashule ya sekondari ya Finland, wavulana na wasichana banafundishwa jinsi ya kupika chakula, kusafisha nyumba na kutunza nyumba yao muzuri.

## Video ya 6: Huduma ya usalama ya jamii na huduma ya afya huko Finland

## Hii ni video kwa ajili ya bakimbizi benye bameenda kuishi huko Finland

**Je, usalama ya jamii imetengenezwa namuna gani huko Finland?**

- Kama uko na afya muzuri na uko chini ya miaka 65, unatarajiwa kufanya kazi kwa wakati bote na kujisaidia wewe na familia yako na mapato ya kutoka kazini.
- Kila mutu analipa ushuru kutoka kwa mapato yake ili kulipia gharama ya huduma ya bato nyonso.
- Ushuru inatolewa pia kutoka marupurupu ya kijamii.
- Finland ni jamii ya kujali batu ambayo inamaanisha kwamba ikiwa mutu hafanyi kazi, ni mugonjwa, mulemavu au muzee, serikali inapatia yeye mahitaji yake ya musingi.
- Huduma yote ya usalama ya jamii banatoka kwa ushuru.

**Je, ninaweza kupata usalama ya jamii huko Finland?**

- Kama mutu ya kukaa kwa manispaa uko na haki ya usalama ya jamii inchini Finland kama wewe unahitaji. Hii ni pamoja na huduma tofauti ya kijamii na faida ya kijamii katika hali tofauti ya maisha.
- Taasisi ya Bima ya Jamii ya Finland, Kela, banatoa huduma kwa batu bote ba kuishi kwa manispaa katika mambo ya usalama ya kijamii.

**Je, mufumo ya usalama ya jamii banatoa huduma kwa wazee na walemavu?**

- Manispaa iko na jukumu ya musingi ya kutunza wazee na walemavu.
- Manispaa inaweza kutoa mahitaji maalumu ya nyumba kama vile kuingia kama uko na kiti ya magurudumu.
- Huduma ya kibinafsi ya wazee na walemavu inapatikana katika manispaa na katika hospitali kuu.
- Bazazi ya mutoto mulemavu sana banaweza kupata musaada ya pesa ya kusaidia gharama kwa ajili ya mutoto.
- Batoto walemavu banaenda shuleni na kupata musaada maalumu kutoka kwa walimu.

**Je, ni faida ya familia ya aina inatolewa kwa bazazi inchini Finland?**

- Uko na haki ya kutumia huduma ya kliniki ya uzazi wakati ya mimba na baada ya kuzaa.
- Kliniki ya uzazi inaangalia afya yako na afya ya mutoto.
- Wanawake bengi banazala katika hospitali ya hali ya juu.
- Baada ya kuzala mutoto, unaweza kumutunza mutoto nyumbani.
- Wakati huu, musaada ya pesa inapatikana kwa muzazi anayelea mutoto, ambaye anaweza kuwa mama au baba.
- Huko Finland, imekua kitu ya kawaida kwa baba kukaa nyumbani na kubatunza batoto wakati mama anafanya kazi.

**Je, niko na haki ya kutumia huduma ya afya huko Finland?**

- Unapatiwa huduma ya afya ya manispaa sawa na batu ba Finland.
- Upimaji ya afya imeandaliwa kwa bakimbizi bote na familia yao banapofika kwa manispaa yao mupya. Hii itaruhusu wafanyikazi ya afya kuamua kama mutu anahitaji huduma yoyote ya afya.
- Ni muhimu kufata maagizo yako na taarifa ya matibabu wakati ya kusafiri.
- Huko Finland, wataalamu bote ba huduma ya afya na wakalimani chini ya sheria lazima basitoe siri ya batu.

**Je, nitapata huduma ya afya ya namuna gani?**

- Kama mukazi ya manispaa utawekwa ndani ya mufumo ya huduma ya afya ya bato nyonso.

- Huduma ya afya ya bato nyonso banatoa huduma ya musingi ya matibabu, lakini kuna tofauti kazaa ya jinsi huduma hii inapangwa katika manispaa tofauti.
- Huduma ya afya ya batoto banaanzia wakati ba kuzala hadi wakati ba kumaliza shule.
- Maitaji yako kwa huduma yoyote ya afya na huduma maalumu ya afya itachunguzwa na kupelekwa kwa huduma inayofaa ikiwa ni lazima.
- Kama umepata mateso au vurugu, unaweza kupata musaada ya kisaikolojia na aina ingine za usaidizi. Hii huduma inapatikana kwa batu ba kila umri.

**Je, itakuwaje nikikuwa mugonjwa wakati ba kufanya kazi?**

- Kila mutu ya kuishi inchini Finland amefunikwa na bima ya afya ya kitaifa, kutoka kwa muchango kutoka kwa batu bote ba bima na waajiri.
- Ukikuwa mugonjwa au kupata ajali, uko na haki ya kukaa nyumbani, lakini lazima umupatie mwajiri wako hati ya daktari.

**Je, batu banapata huduma ya afya kuhusu mambo yao ya kijinsia?**

- Vituo ya afya na kliniki yao ya uzazi inatoa ushauri wa bure kwa mambo ya kijinsia na uzazi.
- Magonjwa ya zinaa inatibiwa katika vituo ya afya au kliniki maalumu. Vituo ya afya inatoa vipimo vya HIV na dawa ya wagonjwa wa HIV inchini Finland ni bure.

**Je, huduma ya afya ya bato nyonso inashughulikia huduma ya meno?**

- Kama mukazi ya manispaa uko na haki ya kutumia huduma ya meno ya bato nyonso.
- Bakimbizi bote batapitia ukaguzi ya meno na batapata ushauri ya jinsi ya kutunza meno yao kwa mambo ya chakula na usafi.
- Kama daktari yako ya meno atagundua unaitaji utunzaji ya meno au upasuaji, utapata miadi ya hii huduma.

**Je, ninaweza kutumia maagizo yangu ya daktari ya zamani kutoka inchi yangu nikifika Finland?**

- Huko Finland, daktari anaandika dawa ya ugonjwa. Utapata maagizo ya daktari ambayo lazima upeleke kwa duka ya dawa ili kununua dawa yako.
- Kama uko na ugonjwa wa muda murefu, chukua maagizo yako ya zamani kwa miadi ya daktari huko Finland.

Unakaribishwa sana kuanza maisha yako mupya inchini Finland! TERVETULOA!